



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO



29/08/2024

TANGAZO KWA WATUMISHI WOTE WA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAMWINO

Kwa siku za karibuni kumejitokeza watu wanaowapigia simu Watumishi na kujitambulisha kuwa ni Maafisa wakitaja kuwa na vyeo na majina ya Viongozi tofauti tofauti wa ngazi za Mkoa na Halmashauri, ambapo wamekuwa wakiwaambia Watumishi kuwa wanafanya zoezi la uhakiki na kwamba taarifa zao zimekosewa na kuwaambia watafukuzwa kazi na baadae kuwataka wawatumie pesa ili wawasaidie wasifukuzwe.

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji inawatangazia Watumishi wote kuwa makini na kwamba wasitoe taarifa zao kwa watu wasiowafahamu wanaowapigia simu ili kuepuka **KUTAPELIWA**. Aidha mnatakiwa kutoa taarifa Polisi mara mnapopigiwa simu na watu hao ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

Prudence Kaaya-Ching'ole,
Kny: Mkurugenzi Mtendaji (W)

Nakala: Mkurugenzi Mtendaji (W)

**Sub-DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
CHAMWINO DISTRICT COUNCIL
P. O. Box 1126
DODOMA**